

# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI

MKOA WA PWANI:  
SIMU: 023 -2010304  
Fax 023 – 2010317  
Email: [ded.rufiji@pwani.go.tz](mailto:ded.rufiji@pwani.go.tz)  
[rufijidc@pwani.go.tz](mailto:rufijidc@pwani.go.tz)



S. L.P 28,  
UTETE/RUFIFI.

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

Unapojobu tafadhali taja:

Kumb. Na.RDC/F.10/6/116

28 Mei, 2021

# TANGAZO

## NAFASI YA KAZI YA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inakaribisha maombi ya nafasi ya kazi ya muda kutoka kwa wananchi wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo za muda kama ifuatavyo:-

### 1.0 Wakusanya Ushuru ( Revenue Collectors) Nafasi 16

#### 1.1 sifa za muombaji

- Awe na elimu ya kidato cha nne/sita
- Awe amehitimu mafunzo ya stashahada/astashahada kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na serikali katika moja ya fani zifuatazo:-
  - Misitu
  - Wanyamapori
  - Uvubi
  - Kilimo
  - Mifugo
  - Usimamizi wa Fedha

#### 1.2 Majukumu ya kazi

- Kusimamia ukaguzi wa mazao yote ya misitu, kilimo,mifugo na uvuvi
- Kukagua stakabadhi zote za ushuru
- Kukagua Leseni zote za mazao ya kilimo,misitu,mifugo na uvuvi
- Kutoa taarifa ya ukaguzi kwa Mkurugenzi Mtendaji kila siku
- Kuwepo katika eneo la kizua wakati wote

### 2.0 Udereva Nafasi 4

#### 2.1sifa za muombaji

- Awe na elimu ya kidato cha nne/sita
- Awe na leseni ya udereva class A,B,D au E
- Awe na cheti cha mafunzo ya udereva kutoka katika chuo kinachotambuliwa na serikali
- Awe na uzoefu wa miaka mitatu na kuendelea

## **2.2 Majukumu ya Kazi**

- kujaza kumbukumbu za magari kwa usahihi kwenye kitabu cha magari (vehicle logbook)
- kuendesha gari la serikali kwa uangalifu/ umakini,kukagua mara kwa mara kabla na baada ya kuliendesha ili kuhakiki liko salama.
- kutunza vifaa na vipuri viliviyomo ndani ya gari na kutoa taarifa ya ubovu wa gari kwa wakati, service na matengenezo
- kuhakikisha gari ulilokabidhiwa ni safi wakati wote na kwenda safari uliyopangiwa
- kuheshimu maafisa/viongozi wakiwa safarini na ofisini na kutunza siri.
- Kufuata taratibu,sheria,kanuni na miongozo ya usalama barabarani.

## **3.0 Ulinzi nafasi 3**

### **3.1 Sifa za muombaji**

- awe na elimu ya kidato cha nne/sita
- awe amehudhuria mafunzo ya Mgambo , JKT au Zimamoto

### **3.2 Majukumu ya Kazi**

- Kulinda usalama wa jengo mchana na usiku
- Kuhakikisha kwamba milango na madirisha yote yamefungwa ipasavyo mwisho wa saa za kazi
- Kuhakikisha kwamba wageni wote wanaoingia katika eneo la ofisi wanaidhini ya kufanya hivyo.
- Kutoa ushauri wa jinsi ya kuboresho huduma ya ulinzi pahala pa kazi.
- Kuhakikisha mali yoyote ya ofisi inayotolewa mlangoni ina hati ya idhini.
- Kupambana na majanga yote yatayotokea katika sehemu ya kazi kama vile moto na kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika kama vile polisi na zimzmoto.


## **4.0 Masharti ya Jumla**

- Awe Raia wa Tanzania
- Awe na umri wa miaka 21 hadi 45
- Uwasilishwaji taarifa za sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria
- Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano
- Maelezo binafsi (cv)
- Nakala za vyeti vya elimu na mafunzo
- Testimonials, provisional results, statement of results na hati za matokeo kidato cha nne na sita (form IV na VI result slips) **HAVITAKUBALIWA**
- 
- Picha mbili (2) passport
- Cheti cha kuzaliwa
- Majina matatu ya wadhamini

Maombi yatumwe kwa mkono, barua pepe au kwa kutumia anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI  
S.L.P 28  
UTETE/RUFIFI**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **11/06/2021 saa 9:30 alasiri**



Geriad Mgoba  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**RUFIFI**

**Nakala:**

Mbao za Matangazo

*GERIAD MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
HALWAASHAURE YA WILAYA YA RUFIFI*